

MAFUTA YA UPAKO

(ANNOINTING OIL)

**Na Siri iliyoko Katika Nguo , Vitambaa, Leso,
Chumvi Na Maji ya Upako.**

Hakimiliki

© Nabii Mkuu Pd Yohana

Hakizote zimehifadhiwa.

Kamwe hairuhusiwikunakili, kuweka kwenye mtandao, kubadirisha, kutafasiri katika lugha yeyote ile au kuchapisha upya chapisho hili bila idhini ya mwandishi.

Nabii Mkuu Pd Yohana

S.L.P 4016

Mwanza Tanzania

Simu : +255 762 415790+255 759 204 744

Yohanayona3@gmail.com

www.hlcenter.info

ISBN : --- - - - - - - - - - -

Toleo la Kwanza 2019.

Kupigwa chapa na

Josia Pd John

Dar es salaam Tanzania

Simu: +255 758 588 127, +255 693 522 834

Josiajohn735@gmail.com

MAFUTA YA UPAKO

(ANNOINTING OIL)

Mafuta ya upako ni nini ?

Mafuta ya upako ni mafuta yaliyo ombewa yakawekwa wakfu ili yatumike kwa ajili ya ibaad, mafuta yaliyotumika kwa kiasi kikubwa katika biblia ni mafuta ya Zeituni, (*olive oil*).

Katika biblia, kuanzia agano la kale mpaka agano jipya kuna mwendelezo wa matumizi ya mafuta ya upako, mafuta haya ya upako yametumiwa kwa kiasi kikubwa sana katika biblia na biblia inatambua imani ya ufunuo inayotumia vitu kusababisha muujiza kutokea, imeandikwa: "*Kwa hukumu zako vimesimama imara hata leo , maana vitu vyote ni watumishi wako "* **Zaburi 119 : 91**

Biblia kwa kiasi kikubwa inaelezea kwa kina kuhusu matumizi ya mafuta ya upako.